Wikendi ya maombi kwa watoto wanaoshi kwenye hali ngumu duniani tarehe

4-5/06/2011

Pamoja Yohana 17:20-23

Ombi la Yesu Kristo lilikuwa yakwamba watu wamuamini kupitia ujumbe wa upendo, kwamba dunia ingem jua Mungu kupitia kwa umoja wa waumini.
Hii ni Changamoto kwetu tunapofanya Kazi na kuomba pamoja kwa ajili ya watoto wanaoshi kwenye hali ngumu na hatari. Tunapoangalia tofauti zilizoko kati yetu kama watu binafsi na sehemu tunazoweza kuathiri. Maombi haya yanatambua sehemu saba katika jamii na jinsi sehemu hizi zinavyoathiri watoto.

Jamii na Elimu

Hizi ni sehemu mbili kubwa kabisa zinazoathiri maisha ya mtoto na pale ambapo umasikini na kuvunjika kwa jamii kuko mtoto huteseka sana. Kuvunjika kwa familia huleta hasara kubwa sana kwenye jamii hasa kwa njia ya wato kutokuwa na furaha. Pahali ambapo umaskini upo na Elimu pia haipo inakuwa vigumu sana kuvunja duara la umaskini katika jamii.

Methali 1

Pamoja Tunaomba ya kwamba:

- Familia zinazoongozwa na watoto ambao wanajaribu kulinda maisha ya familia pamoja watapewa usaidizi wa kijinsia na pia usaidizi unao onekana.
- Familia zinazo ongozwa na mzazi mmoja has zinazoongozwa na wakinamama ambao wamenyanyaswa nakunyonywa.
- Wapate usaidizi na wapate njia ya kutoka kwenya umaskini.
- Watu maskini wapewa fursa ya kupata Elimu.
- Watoto wapewe Elimu ya kimsingi ambao itagusia mahitaji yao ya kiroho, Afya, Lisho bora na Elimu. Watoto pia wawe na fursa ya kujifunza kazi za mikono na ufundi wa kimaisha.
- Wakristo waliomo kwenyo sekta ya Elimu wataweza kushawishi kwa njia nzuri huku wakionyesha maadili na kanuni za kikristo.

Kiitikio cha kutafakari:

Angalia mahitaji ya kijiji unamoishi, Je kunazo familia ambazo zinahitaji usaidizi? Je kunao watoto ambao wameachwa kuishi kivyao na kijitegemea? Je kunawo watoto wanao hitaji usaidizi wa kielimu ali kimasomo?

Biashara na serekali

Hizi ni sehemu mbili ambazo zinaweza kujenga au kubomoa. Vizazi rijaryo katika mataifa mengi. Tukiwa na takribani watoto milioni 218 kati ya miaka 5-7 wakifanya kazi ya kulazimishwa duniani, kuna ushahidi kuwa ufisadi, usherati na uchoyo vimeingilia kanuni za serekali na Biashara ulimwenguni kote.

Zaburi 89:14.

Pamoja Tunaomba ya Kwamba:

- Wafanyi Biashara ambao wana wasaidia watu wanyonge na wale wanaotoa rasilimali zao kusaidia nao kuwezesha kazi ya ufalme wa mungu kwa watoto wanaishi kwenye hali mbaya watapewa Baraka na watu wengine wataiga mfano wao.
- Biashara nyinginezo nyingi zaidi zitasikia sauti ya watoto wanoishi kwenye hali ngumu kwenye Jamii zao na yakwamba watafanya kitendo cha kusaidia hawa watoto.
- Uadilifu na haki vitapewa nafasi ya kwanza katika mijadala ya Bungeni haswa.
- Viongozi wanaochaguliwa serekalini watakuwa na nia nzuri na watakuwa na Rehema kwa vizazi vijavyo na wale ambao hawajazaliwa.
- Serekali mbali mbali zitaombwa kutimizia masharti waliojiwekea masharti ya maedeleo ya kisasi ya umoja wa mataifa na kwamba kutakuwa na kuongezeka kwa maendeleo hayo ifikapo mwaka wa 2015.

Kiitikio cha kutafakari:

Upendo kati yetu unawezaje kuleta mabadiliko katika Jamii yetu?
Haya yataonekanaje katika serekali za mitaa 7 haya yataonekanaje katika kuitika kwetu kwenye Biashara ndogo ndogo na za mitaa, au Biashara kubwa za kitaifa na jinsi tunavyo shirikiana nao.

Vyombo ya habari, sanaa Burudani

Tumeumbwa katika sura ya mwenyezi mungu na sisi pia tu. Binadamu wanaoweza kuumba. Vyombo hivi vya habari vinaweza kuwa na uwezo wa kulekeza maisha ya watoto wanaoshi katika mazingira ya hatari kwa njia mahususi na hata kuwakomboa.

Kinachochukiza ni kuwa vyombo hivi pia vinaweza kuwaharibi watoto na hatakunyonya. Ukuwaji wa haraka wa mitandao ya mawasiliano na vyombo ya habari vimebadilisha sura na upesi wa mwasiliano .Ijapokuwa vitu hivi ni vizuri vikitumiwa kwa makini vitu hivi pia vinaweza kuwa na hatari kwa watoto wengine wengi.

Mwanzo 1:27

Pamoja Tunaomba Yakwamba:

- Wanaofanya kazi kwenye vyombo vya mawasiliano watumie vyombo hivyo kutangaza mambo yanayoleta uzima na maisha kwa watazamaji na wasikilizaji ili waitikie mwaliko wa kiungu na huruma kwa watoto ulimwenguni na vitu vinavyowakumba.
- Wale wanaofanya kazi kubadilisha mawazo ya kizazi kijacho watapata kibali mbele ya vyongozi.
- Wale walio na nia mbaya watafichuliwa na kupatikana ilii maovu yao yasiwaadhiri watoto na kuharibi maisha yao.
- Eleo na umasusi katika sannaa.
- Vitatumiwe kumutukuza mwenyezi mungu. Ili watoto kuonyesha jinsi mungu alivyo waumba.
- Watu wanaofanya kazi na watoto kwa njia ya ubunifu watapewa mikakapi ya kiroho na mawazo ambayo yata saidia watoto kujifungua kutoka kwenye athari za kuumizwa na kutumiwa kikatili.

Kuitika kwa kima wazo:

Je ni kwa kiwangao gani sisi na watoto wetu tumeathiriwa na sanna na Burudani Je vyote ni vizuri? Je ni vitu gani vizuri tumeona vikitendeka katika maisha yetu na kwenye Jamii kuhusu watoto ambavyo vinastahili kuwekwa kwenye vyombo vya Habari.

Je tunawezaje kupata Habari njema katika vyombo vyetu vya habari vya kiasili. Je tunawezaje kuonyesha umaarufu na kuwapa wengine hasa watoto motisha ya kufunya vite.

Dini

Kuna fursa kubwa kanisa kuangaza mwanga katika shawishi hili kwa njia nzuri. Ni katika schemu hii ambapo tunaweza kuonyesha mfano wa yesu Kristo na upendo wake na pia kuonyesha nguvu zake zinazoleta mabadiliko tunapofanya kazi pamoja.

Kuna makanisa 250,000 katika sehemu zilizoathirika sana na ugonjwa wa ukimwi katika mashariki na kusini mwa bara la Afrika haya makanisa yanaweze vizuri kuwahudumia mayatima milioni 12.

Yakobo 1:27.

Tunawomba pamoja yakwamba:

- Wakristo watakuwa katika mustari wa mbele katika kushawishi na wawe sauti ya haki kwa niaba ya watoto.
- Makanisa ya kijamii yawe kielelezo cha upendo wa mwenyezi mungu katika Jamii zao hasa katika kutekeleza mahitaji ya watoto karibu na milango ya makanisa haya.
- Makanisa yawe na mawazo nia moja kuwahudumia watoto jinsi yesu angefanya.
- Watoto wawe mifano ya upendo wa mwenyezi mungu na wawe viongozi wanaomti mungu.
- Watoto wachukue nafasi yao sambamba na watu wazima kama wafanyi kazi katika ufalme wa Mbinguni.

Kuitikia kwa kimawazo:

Je tutawezaje kuambatana na changamoto hii ya kuishi na kufanyakazi na watu wengine walio wa dini tofauti. Tunapojitahidi kuwatunza watoto ni lazima tuweze kupima tumaini tulionayo ndani yetu na kwa unyenyekevu.

Maombi ya Yesu katika Yohana 17 yali jaa tumaini kuwa ulimwengu utajua upendo wa mungu kupitia utukufu wa mungu unaojionyesha maishani mwetu. Hii ndio changamoto yetu kutembea katika utukufu wa Bwana na kwa kumutii.

Kwa kujua mengi zaidi na usaidizi Angalia mtandao: www.viva.org